KUMB: PPR/18 - 07/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 4 JULAI 2018

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 4 Julai 2018.** Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchini, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Juni 2018. Kwa upande wa Mafuta ya Taa, bei za jumla na rejareja hazijabadilika kwa sababu hakuna shehena mpya ya mafuta hayo iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam kwa mwezi wa Juni 2018. Kwa mwezi Julai 2018, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 126/lita (sawa na asilimia 5.53) na Shilingi 166/lita (sawa na asilimia 7.66), sawia. Vilevile, ukilinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli nazo zimeongezeka kama ifuatavyo; Shilingi 125.82/lita (sawa na asilimia 5.83) na Shilingi 165.19/lita (sawa na asilimia 8.10), sawia. Kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la ndani kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuendelea kupanda kwa bei za mafuta hayo kwenye soko la dunia.

(b) Kwakuwa hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga katika mwezi wa Juni 2018, bei za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa Mikoa ya Kaskazini zitaendelea kuwa kama zilivyokuwa katika mwezi wa Juni 2018. Vilevile, kutokana na mkoa wa Tanga kuishiwa Mafuta ya Taa, wamiliki wa vituo vya mafuta katika Mikoa ya Kaskazini wanashauriwa kununua mafuta hayo katika mkoa wa Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa Mikoa ya Kaskazini zitatokana na gharama za mafuta hayo yaliyopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.

(c) Ifahamike kwamba shehena zote za mafuta ya Petroli na Dizeli (kasoro shehena moja) zilizopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam mwezi Juni 2018 zilinunuliwa kwa bei ya mafuta ya soko la dunia ya mwezi Mei 2018 wakati zile zilizopokelewa mwezi Mei 2018 zilinunuliwa kwa bei ya soko la dunia ya mwezi Machi 2018. Hivyo, ongezeko la bei za mafuta nchini katika mwezi wa Julai 2018 limetokana na ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia kwa miezi miwili mfululizo ya Aprili 2018 na Mei 2018.

(d) Kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuanza kupokea mafuta ya petroli kupitia bandari ya Mtwara kwa kutumia Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja (*Bulk Procurement System- BPS*) kwa lengo la kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa mafuta hayo katika mikoa ya kusini (Mtwara, Lindi na Ruvuma), Umma unajulishwa ya kwamba, tarehe 3 Juni 2018, kwa mara ya kwanza, Bandari ya Mtwara ilipokea meli ya mafuta ya Petroli na Dizeli kupitia mfumo wa BPS kwa ajili ya matumizi ya mkoa wa Mtwara. Hivyo, bei za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mkoa wa Mtwara, zimekokotolewa kwa kuzingatia gharama halisi za mafuta hayo yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara na gharama ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika wilaya zote za mkoa wa Mtwara. Kwa Mafuta ya Taa, bei ya mafuta haya katika mkoa wa Mtwara kwa mwezi Julai 2018, imekokotolewa kutokana na mafuta yaliyopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam na hivyo wamiliki wa vituo vya mafuta katika mkoa wa Mtwara wanashauriwa kununua mafuta hayo katika mkoa wa Dar es

Salaam. Kwa mwezi Julai 2018, bei za rejareja za Petroli na Dizeli kwa mkoa wa Mtwara zimeongezeka kwa Shilingi 32/lita (sawa na asilimia 1.35) na Shilingi 124/lita (sawa na asilimia 5.53), sawia.

(e) Ukokotoaji wa bei za mafuta kupitia bandari ya Mtwara kwa mikoa mingine ya kusini (Lindi na Ruvuma) kwa siku zijazo, utategemea kiasi cha mafuta yanayopokelewa katika bandari ya Mtwara, kama yatatosheleza mahitaji ya mikoa yote.

(f) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za kiganjani kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(g) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(h) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula)* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 269/2018 la mwezi Juni 2018**.

(i) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(j) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	**Bei Kikomo**		
	Petroli (Shs/Lita)	**Dizeli (Shs/Lita)**	**Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)**
Dar es Salaam	**2,409**	**2,329**	**2,192**
Arusha	**2,291**	**2,225**	**2,276**
Arumeru (Usa West)	2,291	2,225	2,276
Karatu	2,309	2,243	2,295
Longido	2,302	2,236	2,287
Monduli	2,296	2,230	2,282

Monduli-Makuyuni	2,301	2,235	2,286
Ngorongoro (Loliondo)	2,375	2,309	2,368
Pwani (Kibaha)	**2,413**	**2,334**	**2,197**
Bagamoyo	2,420	2,340	2,203
Chalinze Junction	2,423	2,344	2,206
Chalinze (Msata)	2,427	2,348	2,211
Kibiti	2,429	2,350	2,213
Kisarawe	2,416	2,336	2,199
Mkuranga	2,418	2,339	2,202
Rufiji	2,436	2,357	2,220
Dodoma	**2,467**	**2,388**	**2,251**
Bahi	2,475	2,396	2,258
Chamwino	2,463	2,383	2,246
Chemba	2,494	2,415	2,277
Kondoa	2,500	2,421	2,284
Kongwa	2,465	2,385	2,248
Mpwapwa	2,469	2,389	2,252
Mtera (Makatopora)	2,486	2,407	2,270
Geita	**2,574**	**2,495**	**2,358**
Bukombe	2,563	2,484	2,347
Chato	2,595	2,516	2,379
Mbogwe	2,612	2,533	2,396
Nyang'hwale	2,589	2,510	2,373
Iringa	**2,473**	**2,393**	**2,256**
Ismani	2,478	2,399	2,261
Kilolo	2,477	2,398	2,261
Mufindi (Mafinga)	2,483	2,404	2,266
Kagera (Bukoba)	**2,624**	**2,545**	**2,408**
Biharamulo	2,599	2,519	2,382
Karagwe (Kayanga)	2,641	2,561	2,424
Kyerwa (Ruberwa)	2,646	2,567	2,430
Muleba	2,624	2,545	2,408
Ngara	2,590	2,510	2,373
Misenyi	2,633	2,553	2,416
Katavi (Mpanda)	2,617	2,537	2,400
Mlele (Inyonga)	2,599	2,519	2,382
Mpimbwe (Majimoto)	2,609	2,530	2,392
Kigoma	**2,640**	**2,561**	**2,424**
Uvinza (Lugufu)	2,652	2,573	2,436
Buhigwe	2,629	2,550	2,413
Kakonko	2,597	2,518	2,381
Kasulu	2,626	2,547	2,410
Kibondo	2,604	2,525	2,388
Kilimanjaro (Moshi)	**2,280**	**2,214**	**2,266**
Hai (Bomang'ombe)	2,283	2,217	2,269
Mwanga	2,273	2,207	2,259
Rombo (Mkuu)	2,297	2,231	2,287
Same	2,267	2,200	2,252

Siha (Sanya Juu)	2,287	2,221	2,272
Lindi	**2,468**	**2,388**	**2,251**
Lindi-Mtama	2,486	2,406	2,269
Kilwa Masoko	2,443	2,363	2,226
Liwale	2,489	2,409	2,272
Nachingwea	2,497	2,417	2,280
Ruangwa	2,498	2,419	2,282
Manyara (Babati)	**2,325**	**2,259**	**2,315**
Hanang (Katesh)	2,335	2,269	2,325
Kiteto (Kibaya)	2,340	2,274	2,326
Mbulu	2,337	2,271	2,327
Simanjiro (Orkasumet)	2,357	2,291	2,347
Mara (Musoma)	**2,587**	**2,508**	**2,371**
Musoma Vijijini (Busekela)	2,628	2,549	2,412
Rorya (Ingirijuu)	2,596	2,517	2,380
Rorya (Shirati)	2,631	2,552	2,414
Bunda	2,578	2,499	2,362
Butiama	2,584	2,505	2,368
Serengeti (Mugumu)	2,633	2,554	2,416
Tarime	2,598	2,519	2,382
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,603	2,524	2,386
Mbeya	**2,516**	**2,437**	**2,299**
Chunya	2,525	2,446	2,309
Chunya (Makongolosi)	2,540	2,460	2,323
Kyela	2,532	2,452	2,315
Mbarali (Rujewa)	2,500	2,421	2,283
Rungwe (Tukuyu)	2,525	2,445	2,308
Morogoro	**2,434**	**2,354**	**2,217**
Mikumi	2,449	2,370	2,233
Kilombero (Ifakara)	2,472	2,392	2,255
Kilombero (Mlimba)	2,494	2,415	2,277
Kilombero (Mngeta)	2,483	2,404	2,267
Ulanga (Mahenge)	2,482	2,403	2,266
Malinyi	2,492	2,413	2,276
Kilosa	2,452	2,373	2,236
Gairo	2,452	2,373	2,236
Mvomero (Wami Sokoine)	2,444	2,365	2,228
Turiani	2,459	2,379	2,242
Mtwara	**2,387**	**2,360**	**2,265**
Nanyumbu (Mangaka)	2,417	2,390	2,313
Masasi	2,397	2,370	2,290
Newala	2,400	2,372	2,297
Tandahimba	2,395	2,367	2,290
Nanyamba	2,395	2,367	2,290
Mwanza	**2,559**	**2,480**	**2,342**
Kwimba	2,595	2,516	2,379
Magu	2,567	2,488	2,350
Misungwi	2,564	2,485	2,348

Sengerema	2,591	2,512	2,375
Ukerewe	2,618	2,539	2,402
Njombe	**2,501**	**2,422**	**2,284**
Njombe (Kidegembye)	2,522	2,442	2,305
Ludewa	2,539	2,460	2,323
Makambako	2,493	2,414	2,277
Makete	2,532	2,453	2,315
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,499	2,420	2,282
Rukwa (Sumbawanga)	**2,582**	**2,502**	**2,365**
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,582	2,502	2,365
Kalambo (Matai)	2,589	2,510	2,372
Nkasi (Namanyele)	2,595	2,516	2,379
Ruvuma (Songea)	**2,532**	**2,453**	**2,316**
Mbinga	2,566	2,486	2,349
Namtumbo	2,562	2,482	2,345
Nyasa (Mbamba Bay)	2,568	2,489	2,352
Tunduru	2,591	2,512	2,375
Shinyanga	**2,538**	**2,458**	**2,321**
Kahama	2,551	2,472	2,335
Kishapu	2,566	2,487	2,350
Ushetu (Nyamilangano)	2,569	2,490	2,352
Simiyu (Bariadi)	2,579	2,500	2,363
Busega (Nyashimo)	2,572	2,493	2,356
Itilima (Lagangabilili)	2,582	2,503	2,366
Maswa	2,571	2,491	2,354
Meatu (Mwanhuzi)	2,578	2,498	2,361
Singida	**2,499**	**2,420**	**2,283**
Iramba	2,512	2,432	2,295
Manyoni	2,484	2,405	2,267
Ikungi	2,495	2,416	2,278
Mkalama (Nduguti)	2,524	2,445	2,307
Songwe (Vwawa)	**2,525**	**2,446**	**2,309**
Songwe (Mkwajuni)	2,532	2,453	2,315
Ileje	2,529	2,450	2,312
Momba (Chitete)	2,534	2,455	2,318
Tunduma	2,529	2,450	2,313
Tabora	**2,563**	**2,484**	**2,346**
Igunga	2,517	2,438	2,300
Kaliua	2,581	2,502	2,365
Ulyankulu	2,575	2,496	2,359
Nzega	2,527	2,448	2,311
Sikonge	2,575	2,495	2,358
Urambo	2,576	2,497	2,360
Uyui	2,563	2,484	2,346
Tanga	**2,234**	**2,168**	**2,238**
Handeni	2,255	2,188	2,218
Kilindi	2,270	2,203	2,252
Korogwe	2,246	2,180	2,231

Lushoto	2,255	2,189	2,241
Mkinga (Maramba)	2,241	2,175	2,253
Muheza	2,239	2,173	2,238
Pangani	2,241	2,175	2,245

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	**Petroli (Shs/Lita)**	**Dizeli (Shs/Lita)**	**Mafuta ya Taa (Shs/Lita)**
Bei Kikomo	**2,284.13**	**2,204.67**	**2,068.52**

Bei za Jumla - TANGA	**Petroli (Shs/Lita)**	**Dizeli (Shs/Lita)**	**Mafuta ya Taa (Shs/Lita)**
Bei Kikomo	**2,109.92**	**2,043.69**	**---**

Bei za Jumla - MTWARA	**Petroli (Shs/Lita)**	**Dizeli (Shs/Lita)**	**Mafuta ya Taa (Shs/Lita)**
Bei Kikomo			**---**

Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA